TANGAZO LA SERIKALI NA. 768 la tarehe 30/8/2024

SHERIA YA PETROLI,
(SURA YA 392)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128(3))*

## NOTISI YA KIBALI CHA UJENZI WA GATI LA KUPOKEA MELI ZA MAFUTA AU GESI NA BOMBA LA KUPOKEA MAFUTA AU GESI KUTOKA KWENYE GATI HADI KWENYE GHALA LA MAFUTA AU GESI KWA KAMPUNI TAIFA GAS TANZANIA LIMITED YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Gati la Kupokea Meli za Mafuta au Gesi na Bomba la Kupokea Mafuta au Gesi kutoka kwenye Gati hadi kwenye Ghala la Mafuta au Gesi kwa Kampuni ya Taifa Gas Tanzania Limited ya Mwaka 2024.

Tafsiri

2. Katika Notisi hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"mwombaji" maana yake ni Taifa Gas Tanzania Limited wa S.L.P 77578, Dar es Salaam;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji; na (Sura ya 414)

"kibali cha ujenzi" maana yake ni kibali kilichotolewa na Mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 128(1) cha Sheria ya Petroli. (Sura ya 392)

Kutolewa kwa kibali cha ujenzi

3. Mwombaji anapewa kibali cha ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa gati la kupokea meli za mafuta au gesi katika eneo lililopo kilomita 1.2 kutoka ufukweni bahari ya Hindi na bomba la kupokea mafuta au gesi lenye urefu wa kilomita 1.2 kutoka kwenye gati hadi kwenye bandari ya

Tanga lililopo Kiwanja Na. 64, Kitalu "A", Kijiji cha Ndaoya na Putini, Kata ya Chongoleani, Mkoa wa Tanga, kwa masharti yafuatayo:

(a) gati la kupokea meli za mafuta au gesi na bomba la kupokea mafuta au gesi litajengwa kwa kuzingatia viwango vikiwemo viwango vya Shirika la Viwango vya Kimataifa ISO 19901-7:2013, Viwango vya Taasisi ya Petroli ya Marekani API RP 2SK na API 570, Viwango vya Det Norske Veritas DNV-OS-E403, Baraza la Majini la Kampuni za Mafuta la Kimataifa, muongozo na mapendekezo, teknolojia na misingi ya uhandisi na mienendo bora ya ufanyaji shughuli za petroli inayokubalika kimataifa;

(b) gati la kupokea meli za mafuta au gesi litajengwa likiwa na uwezo wa kuhimili matukio ya mabadiliko ya hali ya hewa ikiwemo mawimbi, upepo mkali, mkondo, kimbunga, uzito wa meli na dhoruba zinazotokana na mabadiliko ya misimu;

(c) nyaya za kuunganisha meli na gati la kupokea meli za mafuta au gesi zitakuwa na uwezo wa kuhimili uzito wa meli;

(d) gati la kupokea meli za mafuta au gesi litakuwa na nguzo imara ambazo zina uwezo wa kuhimili dhoruba za baharini, uzito wa meli na kuhakikisa shughuli za ufungaji meli katika gati zinafanyika kwa usalama;

(e) kuhakikisha vifaa kwa ajili ya ujenzi wa gati la kupokea meli za mafuta au gesi vitakuwa na uimara wa kutosha na unyumbulifu, visivyoweza kushika moto au kutu kwa urahisi, rahisi kuchomelea, na kuwekwe mifumo yakudhibiti kutu;

(f) kuhakikisha kunakuwa na vifaa vya kupima na kufuatilia mabadiliko ya hali ya hewa kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki za kujikinga na dhoruba zinazotokana na mabadiliko ya hali

ya hewa;

(g) kuhakikisha gati la kupokea meli za mafuta au gesi litakuwa na vifaa vya kutosha vya kukabiliana na moto;

(h) eneo la gati la kupokea meli za mafuta au gesi litakuwa na ukubwa wa kutosha ili kuwezesha meli kuingia na kutoka kwa urahisi na kuhakikisha operesheni zinafanyika kwa ufanisi na usalama;

(i) kuhakikisha kunakuwa na mifumo ya mawasiliano kwa ajili ya gati la kupokea meli za mafuta au gesi na bomba lake kwa ajili ya kufuatilia operesheni za upokeaji mafuta au gesi;

(j) kuhakikisha bomba la kupokea mafuta au gesi lina mifumo ya kulinda na kufuatilia utendaji wake ikiwemo mifumo ya kuzuia kutu, vali za kupunguza shinikizo la mafuta au gesi kwenye bomba, vali za kufunga bomba, geji za kupima shinikizo la mafuta au gesi, alama zinazoonesha mkuza wa bomba, mfumo wa kugundua uvujaji wa mafuta au gesi, na mfumo wa kusafisha na kufuatilia hali ya ubora wa bomba; na

TS. Na. 197 la 2017

(k) atahakikisha kampuni pamoja na wakandarasi wote wanazingatia masharti ya Kanuni za Mafuta ya Petroli za Ushirikishwaji wa Wazawa.

Ukomo wa kibali cha ujenzi

4. Kibali cha ujenzi kitakoma au kuisha muda wake endapo ujenzi wa gati la kupokea meli za mafuta au gesi na bomba la kupokea mafuta au gesi hautaanza ndani ya miezi ishirini na nne kutoka tarehe ya kutolewa kwa kibali hiki.

Dodoma,
…………………, 2024

JAMES A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*